

**MKATABA WA KUPANGA ENEO LA BIASHARA YA YARD YA MAGARI**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe -----siku ya -----mwaka 2024

**KATI YA**

**SIMBA DEVELOPERS LIMITED** wa S.L.P 2562 Dar es Salaam (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "mwenye ENEO") kwa upande mmoja.

**NA**

**MACHO ENERGY COMPANY LIMITED** wa S.L.P 110233 Dar es Salaam, ambayo ni kampuni binafsi anayefanya biashara ya usafirishaji, vituo vya mafuta na gesi kwa njia ya barabara ambapo katika mkataba atatambulika kama "MPANGAJI" kwa upande mwingine.

**AMBAPO MWENYE ENEO** ni mmiliki halali wa eneo lililopo kidongo chekundu KURASINI karibu na africab bulding

**KWAHIYO**, MWENYE ENEO bila ya kulazimishwa na mtu yeyote na akiwa na akili zake timamu ameamua kumpangisha MPANGAJI sehemu ya eneo lake la yard lenye utambulisho hapo juu ambalo linaweza kukaa MAGI ZAID YA 120 aina ya marori ya mafuta MWENYE ENEO ameridhia MPANGAJI alipe kodi ya upangaji wa eneo analolitumia kwa kiasi cha Shilingi za kitanzania **million moja Tu kwa Mwezi(Tshs. 3,000,000/=)** na kufanya kodi ya upangishaji kwa miaka 6 kuwa Tshs. 216,000,000/= tu.

**HIVYO BASI, MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:**

- 1. MPANGAJI** atakuwa na wajibu wa kumlipa mwenye ENEO kodi ya upangaji kila baada ya miaka 3 na malipo hayo yatafuata utaratibu ufuatao;
  - (i)** Tarehe 01/01/2024 mpangaji atamlipa mwenye eneo kiasi cha **Shilingi milioni mia na nane tu( Tshs. 108,000,000/)**
  - (ii)** Tarehe 01/01/2026 mpangaji atamlipa mwenye eneo kiasi cha **Shilingi milioni mia na nane tu( Tshs. 108,000,000/)**
- 2. Mwenye eneo** atahusika na malipo yeyote ya mkataba huu, gharama nyingine zitalipwa na mpangaji.
- 3. Mpangaji** atawajibika na ulinzi wa eneo alilokodishwa na kwamba anaweza kuwa na walinzi wake binafsi

**4. Mkataba huu utaongozwa na kutawaliwa na Sheria za Tanzania**

**KWA USHUHUDA** wa makubaliano hayo pande zote mbili zimetia sahihi kama ilivyo hapa chini;

UMETIWA SAHIHI na kutolewa na  
**Simba developer limited** ambaye  
namfahamu/ametambulishwa kwangu na  
.....leo tarehe 01 mwezi 01..  
mwaka 2024.



**MWENYE ENEO**

**MBELE YANGU**

Jina: ADVENTINA G. MAGALA

Sahihi: AS

Anuani: S.L.P 33142

Kazi/wadhifa: WAKILI



UMETIWA SAHIHI na **KHALID WAHID ABEID AWADH**  
Ambaye ni mpangaji  
namfahamu/ametambulishwa  
kwangu



**MKODISHWAJI**

...01/01/2024...leo tarehe ..... mwezi .....  
mwaka 2024.

**MBELE YANGU**

Jina: ADVENTINA G. MAGALA

Sahihi: AS

Anuani: S.L.P 33142

Kazi/wadhifa: WAKILI



**Umeandaliwa na;**

**Wahusika**

**Dar es Salaam.**